

Abiria wakiwa katika foleni ya kupanda mwendokasi katika Kituo cha Mbezi Mwisho jijini Dar es Salaam jana. **Picha na Said Khamis**

Mwananchi Jumanne Septemba 30/2025 pg 9

CamScanner

Web: www.jamhurimedia.co.tz : Jamhuri DIGITAL

# JAMHURI

Bei Tsh 1,000

JAMHURI Jumanne Septemba 30 - Oktoba 6, 2025 ISSN No 1821-8156 Toleo No. 733

Tunaanzia Wanapoishia Wengine

291

# SGR kutua Mtwara

- Kuziunganisha bandari za Mtwara, Mbambabay; Tanzania, Malawi
- Itarahisisha usafirishaji chuma, makaa ya mawe kutoka Liganga, Mchuchuma



- Uchumi wakadiriwa kupaa kutoka Dola bilioni 85 hadi Dola bilioni 135
- Tanzania kuwa na mtandao mrefu zaidi wa SGR Afrika, ukiunganisha nchi tatu





Rais Samia Suluhu Hassan

SOMA UK. 2

CS CamScanner

# SGR kutua Mtwara

**MTWARA**

MWANDISHI **WETU**

Mipango ya serikali kuongeza mtandao wa reli ya kisasa (SGR) nchini imo katika hatua za mwisho; JAMHURI linaripoti.

Ujenzi wa vipande (lots) sita vya SGR ushoroba wa kati kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza, Kigoma na Musongati nchini Burundi umo katika hatua mbalimbali; huku huduma ikitolewa katika 'lots' mbili za mwanzo, Dar es Salaam hadi Dodoma.

Mtandao wa SGR Tanzania utakapokamilika unatarajiwa kuyaunganisha mataifa ya Tanzania, Burundi na DRC.

Akizungumza na wananchi wa Mtwara wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu 2025, mgombea urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Samia Suluhu Hassan, amesema ndani ya miaka mitano ijayo ujenzi wa reli ya kisasa yenye urefu wa kilomita 1,000 ukanda wa kusini mwa Tanzania utaanza.

"Tumekaa na mjenzi (mkandarasi). Kuna mambo alisema turekebishe, tumefanya hivyo. Sasa tuko kwenye mazungumzo mengine. Reli (hii) itapita maeneo yenye utajiri mkubwa wa mazao ya nafaka na kuunganisha (Bandari ya Mtwara na) maeneo ya Liganga na Mchuchuma," amesema Dk. Samia ambaye pia ni Rais wa Tanzania.

Ujenzi wa SGR kutoka Mtwara hadi Mbambay, Nyasa mkoani Ruvuma utafungua ukurasa mpya wa maendeleo ya miundombinu kwa mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma yenye utajiri mkubwa wa rasilimali.

Miongoni mwa bidhaa zinazotarajiwa kusafirishwa mbali na abiria ni gesi, makaa ya mawe kutoka Liganga na chuma kutoka Mchuchuma.

**Historia ya reli kusini mwa Tanzania**

Katika miaka ya 1940, Serikali ya kikoloni chini ya Uingereza ilianzisha ujenzi wa reli kutoka Mtwara hadi Nachingwea, maalumu kwa ajili ya mradi wa karanga (Tanganyika Groundnut Scheme).

Gavana wa Tanganyika, Sir Edward Twining, alikuwa mgeni rasmi wakati wa uzinduzi wa safari ya kwanza ya treni katika reli hiyo mwaka 1949, iliyolenga kusafirisha shehena ya karanga na wafanyakazi; akiahidi kuwa ule ulikuwa mwanzo tu wa maendeleo makubwa ya miundombinu na uchumi wa kusini mwa Tanganyika (sasa Tanzania).

Ikumbukwe kuwa, baada ya Vita Kuu ya Pili ya dunia, Uingereza ilikumbwa na uhaba mkubwa wa mafuta ya kula hivyo Nachingwea ikatarajiwa kuwa mkombozi.

Hata hivyo, kutokana na changamoto mbalimbali, mradi huo ulifeli na baadaye reli ikang'olewa na kubaki kuwa alama ya kihistoria, na sasa Serikali ya Awamu ya Sita imepania si tu kufufua historia ya matumaini, bali kujenga reli bora zaidi kuliko ya awali iliyokuwa nyembamba



Rais Samia Suluhu Hassan.

(narrow gauge railway) na kuwa SGR.

**Uchumi wa Tanzania kupaa**

Uamuzi wa serikali kujenga SGR kusini mwa Tanzania unapanua mtandao wa reli hiyo kutoka zaidi ya kilomita 2,000 za sasa na kufikia zaidi ya kilomita 3,000; hivyo kuwa taifa lenye mtandao mpana zaidi barani Afrika.

Reli hiyo itachagiza kukua kwa uwekezaji uliofanywa Liganga na Mchuchuma ambako walau Dola za Marekani bilioni 3 sawa na zaidi ya Sh trilioni 7.3 zimewekezwa; huku pia kukiwa na uwekezaji wa Dola za Marekani bilioni 42 sawa na Sh trilioni 102,76 kwenye mradi wa gesi ya LNG mkoani Lindi.

Takwimu zinaonyesha kuwa hadi mwaka 2024 uchumi wa Tanzania ulikuwa ni Dola za Marekani bilioni 85.42 sawa na Sh trilioni 209.0.

Kutokana na uwekezaji unaowezeshwa na Serikali ya Awamu ya Sita kupitia sekta binafsi na sekta ya umma sambamba na ahadi za Dk. Samia, wataalamu wa uchumi wanakadiria kuwa uchumi wa Tanzania utafikia Dola za Marekani bilioni 135 sawa na Sh trilioni 330.3 ifikapo mwaka 2027.

Makadirio hayo yakienda sambamba na ujenzi wa mtandao wa SGR, miradi ya LNG, Liganga, Mchuchuma, Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP – Dola za Marekani bilioni 5.65) na mingine mingi ya kimkakati, yatauweka uchumi wa Tanzania juu ya Kenya, ambao kwa sasa uchumi wake ni Dola za Marekani bilioni 110, sawa na Sh trilioni 269.1.

Dk. Samia anasema mradi mkubwa wa LNG umo katika hatua za mwisho za makubaliano na mwekezaji; majadiliano yanalenga kuhakikisha kila upande unanufaika.

"Mwekezaji yeyote akiwekeza lazima awe na uhakika, na sisi tuwe na uhakika tutapata nini kutoka kwenye rasilimali yetu… Tumezungumza sana, nawaambia tupo hatua za mwisho za makubaliano.

"Baada ya kukubaliana tutasaini mkataba. Ninachotaka kuwaambia mradi upo, usingekuwa na manufaa bila kufanya mazungumzo mpaka tuelewane, tujue tunapata nini na wao wanapata nini," anasema.

Takwimu zinaonyesha Tanzania inakadiriwa kuwa na futi za ujazo trilioni 57, kati ya hizo trilioni 49 zimo ndani ya Bahari ya Hindi.

Mkoa wa Ruvuma una madini ya vito, makaa ya mawe na dhahabu, yamekuwa kichocheo kikubwa cha uchumi, yakiingiza maduhuli ya serikali hadi kufikia asilimia 98 ya lengo mwaka 2024/25.

Hadi Mei 19, 2025 mkoa huo ulikuwa umekusanya Sh bilioni 32.5 kati ya lengo la kukusanya Sh bilioni 33.15.

Makaa ya mawe sasa yanauzwa Kenya, Malawi, Rwanda, Uganda, Ulaya na Asia.

Mradi mwingine ulioahidiwa na Dk. Samia ni ujenzi wa mtandao wa barabara zote zinazounganisha bandari za Mtwara na Mbambabay kwa kiwango cha lami ndani ya miaka mitano ijayo.

Barabara hizo ni Mnivata - Masasi (kilomita 160) na Daraja la Mbiti; Dar es Salaam – Kibiti – Lindi – Mingoyo (kilomita 487) ambayo kazi ya ujenzi inaendelea katika maeneo mbalimbali.

Ufanisi wa Bandari ya Mtwara umeongezeka kutoka kuhudumia shehena tani 40,000 hadi tani 110,000 kwa mwaka na abiria kutoka 45,000 hadi 100,000.

"Bandari na reli hizi ni mkakati katika usafiri na kusafirisha mizigo na watu, ndiyo maana tunakuja na ujasiri mkubwa wa kufanya mambo makubwa haya," amesema Dk. Samia.

Akiwa mkoani Lindi, Dk. Samia amehidi kujenga Uwanja wa Ndege wa Lindi Kusini, akisema tayari fedha zimeshapatikana.

Kukamilika kwa uwanja huo kutasaidia kupunguza adha kwa wananchi wanaolazimika kusafiri kilomita 100 hadi Mtwara kufuata huduma ya ndege.

**Wadau**

Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Sera za Kiuchumi (TICGL), Dk. Amran Bhuzohera, amesema uamuzi wa Rais Samia kujenga reli hiyo ni hatua muhimu kwa uchumi wa taifa.

"Kama mradi huu utakamilika, Tanzania itakuwa kitovu cha usafirishaji na biashara katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, itasaidia kuongeza pato la taifa na wananchi wote ambao wako ukanda huo.

"Mafanikio haya yatategemea usalama wa ujenzi, uajibikaji wa kifedha na uwazi wa serikali, kiuchumi jambo hili limekaa vizuri sana, pato litakua, ajira zitaongezeka na biashara itapanuka," amesema.

Amesema lazima serikali iwajibike kwa umma, iweke usalama na kuhakikisha miradi inajengwa kwa viwango vya juu, mradi ukamilike kwa wakati. Naamini uchumi wa mikoa ya kusini unaweza kukua kwa wastani wa asilimia 5-7 kwa mwaka miaka michache ijayo.

Mchumi nguli wa masuala ya biashara, Dk. Bravious Kahyoza, amesema ujenzi wa reli hiyo utafungua fursa nyingi za uchumi, si kwa kanda hiyo tu, bali taifa zima.

Kuhusu maeneo ya pembezoni na ya kati ndani ya nchi, anasema: "Ni vizuri kutatua changamoto kubwa za aina hii kupitia ugatuaji ambao unalenga kuimarisha miundombinu kila pembe ya nchi."

Anasema ahadi ya Rais Samia inaibua masuala muhimu katika Dira ya Taifa ya Maendeleo, tayari hatua zimeanza kuchukuliwa ili kufikia malengo ya 2050.

"Utekelezaji wa ahadi hii utakuwa na matokeo chanya kwa uchumi wa watu wa mikoa ya kusini, ukizingatia wengi wao wanajihusisha na kilimo. Siku zote serikali inapoimarisha huduma za miundombinu ya reli inachochea shughuli za uchumi na kuimarisha masoko, hivyo kurahisisha usafirishaji wa bidhaa katika mikoa hiyo kwenda sokoni kwa wakati," amesema.



Mgombea wa urais Dk. Samia Suluhu Hassan akimkabidhi Ilani ya Uchaguzi ya CCM, Mgombea Ubunge wa Jimbo la Mchinga Salma Kikwete.

CamScanner